

# MKATABA WA UPANGAJI

MKATABA huu umetayarishwa leo tarehe 03 mwezi O I .mwaka 2025

## KATI YA

NEEMA CHARLES wa Dar es salaam Tanzania (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "MWENYE NYUMBA") kwa upande mmoja.

YANGTZE TANZANIA ENTERPRISE LIMITED wa Dar es salaam (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "MPANGA.JI" kwa upande mwingine.

NA KWA VILE Mwenye NYUMBA amekubali kupangisha na Mpangaji amekubali kupangishwa sehemu ya nyumba (Chumba) hiyo iliyopo ILALA Mtaa wa MATUMBI kata ya TABATA, Namba ya nyumba 56, Block B, Hot no 56

HIVYO BASI Makubaliano hayo yameshuhudia yaftatayo:-

### 1. MUDA WA MKATABA

Mkataba huu utakuwa wa kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe 03 Mwezi OI mwaka 2025 na utamalizika tarehe 02 mwezi OI mwaka 2030.

### 2. KODI

Mwenye nyumba amekubali kupangisha na mpangaji amekubali kupangishwa katika sehemu hiyo ya nyumba kwa madhumuni ya kufanya biashara kwa kulipa kodi ya shilingi Milioni Mbili Tu ~~000,000~~ kwa mwezi mmoja. Wakati wa kutiliana Saini mwenye nyumba amekubali kupokea Tsh

Milioni Ishirini na Nne Tu ~~24,000,000~~ Ikiwa ni malipo ya mwaka mzima.

### 3. NI WAJIBU WA MPANGA.JI KUTEKELEZA YAFUATAYO:-

- (a) Kutopangisha Mtu mwingine katika nyumba hiyo bila idhini ya Maandishi ya Mwenye nyumba
- (b) Kulipia gharama zote za umeme katika chumba hicho kwa kipindi cha Mkataba.

- (c) Kuweka chumba na mazingira yake katika hali ya usafi na kufanya matengenezo madogo madogo inapobidi na gharama za matengenezo kvva matumizi yake hazitakuwajukumu la Mwenye nyumba
- (d) Iwapo makubaliano hayo hayataongezwa muda wake, atamkabidhi Mwenye nyumba sehemu hiyo ikiwa tupu-

4 NI WAJIBU MWENYE NYUMBA KUTEKELEZA YAFUATAYO: -

- (a) Kuweka nyumba katika hali nzuri
- (b) Kutombughudhi Mpangaji wa chumba hieho anayesimamia kwa masharti yaliyopo.

5. INAKUBALIWA PIA KUWA

- (a) Endapo Mpangaji atakuwa na Nia ya kuendeleza atawajibika kutoa taarifa ya Maandishi ya mwezi mmoja kabla ya kipindi cha Mkataba kuisha.
- (b) Kama Mpangaji hatakabidhi nyumba hiyo kama walivyokubaliana basi Mwenye nyumba ana haki ya kumtoa lava kutumia Dalali yeyote bila amri yoyote ya Mahakama.
- (c) Mgogoro wowote utatokea kuhusiana na Mkataba huu, basi mgogoro huo utatambuliwa kufuatana na sheria za nchi-

Mkataba huu uneshuhudiwa na wahusika kwa kutia sahihi zao katika namna na katika tarehe, mwezi na mwaka unaoonekana hapa chini.

UMESAINIWA na KUTOLEWA na  
NEEMA CHARLES ambaye amekubaliwa Na  
ambaye namfahamu hapa Dar es salaam Leo 03  
mwezi 01 mwaka 2025.

}   
.....  
MWENYE NYUMBA

W.H.T - 2400,000/=  
SLURRY - 240,000/=  
TOTAL 2640,000/=

UMESAIMWA na KUTOLEWA  
Na YANGTZE TANZANIA ENTERPRISE  
sLIMITED ambaye amekubaliwa  
Na ambaye namfahamu hapa Dar es salaam  
Leo 03 mwezi 01 mwaka 2025.



)  
.....

MPANGAJI

SHAHIDI;

JINA DANIEL SIMON  
SAHIHI   
ANWANI 105269, D/M  
KAZI WAKILI



STAMP DUTY  
Shs 240,000/- Collected  
Receipt No 9984119765499  
Date 6/01/25  
Regional Manager